# MWONGOZO MFUPI WA UANDISHI

Mara kadhaa vijana wenye ndoto ya kuandika huniuliza nama ya kuwezesha ndoto yao kufaulu. Naoredhesha hatua nane ambazo, kwa maoni yanyu, zikifuatwa kwa makini, zinaweza kusafirisha mtu kutoka kiwango za kuwa na ndoto ya kuwa mwandishi hadi kufikia kiwango cha kuwa mwandishi haswa.

HATUA YA KWANZA: Chombo muhimu kabisa cha mwandishi ni lugha. Ni kazi bure kujaribu kuandika fashihi wakati mtu hana lugha ya kutosha na inayofaa. Kwa hivyo, hatua ya kwanza kwa anayetaka kuwa mwandishi ni kuimarisha lugha, kwa mfano, kwa kusoma vitabu na magazeti, kusikiliza redio na televisheni, na kuwa na mazoa ya kutumia vizuri lugha. Kuna watu ambao tayari wana ukwasi wa kutosha wa lugha kutokana na amali yao. Kwa mfano, kama mtu amekuwa mtangazaji wa televisheni au redio kwa muda mrefu; kama mtu amekuwa mwandishi wa magazeti kwa miaka mingi; au kama amekuwa akisoma vitabu vya fasihi na kuifundisha kwa muda mrefu, labda mtu huyo atakuwa amehitimu kiwango cha lugha kitakachomwezesha kuwa mwandishi. Kwa hivyo, anaweza kuanza kupalilia ndoto yake ya uandishi kwenye Hatua ya Pili.

HATUA YA PILI: Uandishi unahitaji stadi maalum. Kwa mfano, kuna mbinu maalum za kuunda wahusika katika riwaya au tamthilia; lugha ya wahusika katika tamthilia ina sifa mahsusi; tamthilia ina muundo unaoitenga na riwaya, ushairi, hadithi fupi, tawasifu, wasifu na kadhalika; na lugha inayotumiwa na waandishi ina sifa zinazoipa upya, kina na ladha ikilinganishwa na lugha ya kawaida. Anayetaka kuwa mwandishi, hana budi kujifunza sifa na mbinu za utanzu wa fasihi anaotaka kuandikia na vilevile mikakati ya lugha ya kifasihi. Kama nilivyosema kuhusu Hatua ya Kwanza, kuna uwezekano kwa mtu kuwa amefikia Hatua ya Pili bila kufanya bidii kimaksudi. Kwa mfano, ikiwa mtu amesoma mashairi mengi sana, atakuwa amegundua jinsi shairi linavyopangika, namna washairi wanavyofinyanga lugha na labda masuala yanayostahili kushughukiwa katika ushairi. Mtu kama huyo anaweza kuwa tayari amepata stadi za kuandika ushairi. Hivyo hivyo kwa mtu ambaye amesoma tamthilia nyingi; amezoea kwenda theata kutazama uigizaji wa michezo na ametazama maigizo mengi ya michezo. Mtu kama huyo huenda akawa amepata stadi zinazotumika katika kuandika michezo bila yeye kujifunza mbinu hizo kimaksudi.

HATUA YA TATU: Ili kuandika kazi nzuri ya fasihi, inabidi mwandishi aelewe vizuri suala au jambo analonuia kuandikia. Kwa sababu hii, ni muhimu mtu kujiuliza kama ana habari za kutosha kuhusu suala analotaka kushughulikia katika shairi, riwaya, tamthilia, hadithi fupi na kadhalika. Ikwa hana habari za kutosha, inabidi achunguze au afanyie utafiti uala hilo. Kwa mfano, kwa miaka mingi, nimekuwa na hamu ya kuandika tamthilia kuhusu dawa za kulevya miongoni mwa vijana. Tatizo langu kubwa ni kwamba, kwa hivi sasa, sina habari za kutosha kuniwezesha kuandika tamthilia hiyo. Siwezi kutofautisha athari za kokeni kutoka zile za heroini. Sijui tofauti ya jinamizi zinazotokana na bangi na zile zinazoletwa na Mandrax. Sijui kama kuna tofauti baina ya tabia ya msichana na ya mvulana baada ya kutumia dawa za kulevya. Kuna uwezekano mkubwa kwamba nitaandika tamthlia kuhusu dawa za kulevya. Hata hivyo, kabla ya kuandika mchezo huo, itanibidi nitanye utafiti. Itabidi, labda, nitafute habari kwenye

mtandao, kwenye vitabu na magazetini. Itabidi, labda, nizungumze na madaktari wa akili, wanasaikolojia na wauguzi ambao wanafanya kazi katika asisi za wagonjwa walioathiriwa na dawa za kulevya. Itabidi, labda, nizungumze na vituo vya kurekebisha waathiriwa wa dawa za kulevya. Hata huenda nikatafuta kibali kuingia kwenye vituo vya kurekebisha waathiriwa wa dawa za kulevya.

HATUA YA NNE: Hii ni hatua ya kuandika yale ambayo mwandishi amekusudia kuandia. Inabidi mtu amue utaratibu wa kuandika. Anaweza kutenga saa au siku maalum za kuandika.Kwa mfano, anaweza kupanga kuandika kuanzia saa kumi alasiri hadi saa mbili usiku kutoka Jumatatu hadi Ijuamaa.
Anaweza kutenga Ijumaa na Jumamosi kuwa siku za kuandika pekee. Anaweza kutenga wiki au miezi kadhaa ambapo kazi yake itakuwa kuandika tu. Ni muhimu kutaja kwamba kutenga wakati wa kuandikia si jambo gumu. Ugumu umo kwenye kutekeleza uamuzi huo. Watu wengi hawana nidhamu na stahamala za kutekeleza uamuzi wao. Kama unataka kuwa mwandishi, huna budi kujishawishi kuwa na hali ya juu kabisa ya nidhamu ikiwa ni pamoja na kuwa tayari kujinyima starehe kwa madhumuni ya kuandika hadi kukamilisha kazi.

HATUA YA TANO: Baada ya kuandika kazi nzima, ni muhimu kuipitia na kuirekebisha. Marekebisho hayo ni ya aina nyingi. Kutakuwa na sehemu za kukata na kuondolea mbali; sehemu za kuongeza; mapengo ya kujaza; wahusika wa kuunda upya au kutupilia mbali; Kupeleka mbele, katikati au nyuma sehemu fulani ili kuboresha msuko (au ploti); kuimarisha maudhui ya kazi; kuboresha taharuki; kurekebisha usimulizi; na kadhalika. Marekebisho hayo si jambo la kufanya mara moja tu. Waandishi wanaoishia kuwa na kazi nzuri huwa na mazoea ya kurekebisha kazi zao mara nyingi.

HATUA YA SITA: Baada ya kuridhika na marekebisha, ni vizuri mwandishia kuwapa watu kazi yake ili waisome na kumpa maoni. Baadhi ya wale ambao wamekuwa wakiniandikia wakitaka niwape mawaidha kuhusu uandishi ni vijana wa vyuo vikuu na wa shule za upili. Katika vyuo vikuu na shule za upili kuna walimu wa fasihi. Mwanafunzi anaweza kumwomba mwalimu wa fasihi aisome kazi yake ili ampe mashauri. Wale ambao hawamo katika asisi za masomo wanaweza kumpa yeyete mwenye ujuzi wa fasihi kazi zao ili wapate maoni.

HATUA YA SABA: Baada ya kupata maoni kuhusu kazi ya fasihi, ni muhimu kuyatilia maanani maoni hayo. Si vizuri mwandishi kuwa na kiburi au kufikiria kwamba akili yake ni bora kuliko akili za watu wengine. Ikiwa maoni iliyopata mwandishi yanamulika udhaifu katika kazi, ni muhimu kuondoa udhaifu huo bila kukasirika au kuona haya kwamba amekosolewa. Kuwa mwandishi si kuwa malaika; mwandishi ni binadamu kama binadamu wengine!! Ningepernda nieleweke vizuri. Siyo kila jambo ambalo watu wengine wanaona ni udhaifu huwa udhaifu. Unapoona kwamba ukibadilisha sehemu fulani ya kazi yako utakuwa umepunguza thamani yake au kubadilisha lengo lako la kuiandika kazi hiyo, ni bora kutotekeleza pendekezo au mapendekezo yanayokutaka kuibadilisha kazi.

HATUA YA NANE: Sasa ni wakati wa kupeleka kazi yako kwa kampuni ya uchapishaji. Unapofanya hivyo, hakikisha kwamba umebaki na nakala ya kazi yako.

VIJANA, MSIPOANDIKA, MSITOE UDHURU KWAMBA WAZEE WALIWANYIMA MAWAIDHA YA KUWAONGOZA!!